

## HATIFUNGANI YA KIJANI SASA YAORODHESHA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM

**27.10.2023** ilikua moja ya siku ya kipekee sana ambapo Soko la Hisa la Dar es salaam liliorodhesha Hatifungani ya Kijani "**GREEN BOND**" ya benki ya CRDB ambayo ni hatifungani ya kwanza ya aina hiyo kuorodheshwa na kufanya benki hiyo kuweka historia ya kuwa taasisi ya kwanza nchini na si Tanzania tu bali na nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara kufanya hivyo.

Benki hiyo imefanikiwa kukusanya **Shilingi za kitanzania bilioni 171.82** sawa na **ziada ya 329.55%** kutoka kwa **wawekezaji 1,754** ambapo **lengo likiwa kukusanya bilioni 40**. Hii inaonyesha jinsi gani Soko la Hisa la Dar es salaam linaweza kutumiwa na serikali au taasisi mbali mbali kupata fedha kwa ajili ya kuendesha/kuendeleza miradi lengwa.

Hafla iliyoandaliwa na mwenyeji ambaye ni **Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DSE Madam Mary S. Mniwasa**, **Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa benki ya CRDB Ndugu Abdulmaji Nsekela**, mgeni Rasmi **Dk.Charles Mwamwaja** Kamishna kutoka Wizara ya Fedha, **Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji CPA Nicodemus Mkama** na wawakilishi wa taasisi nyingine za kiserikali na binafsi.



